JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU

# SERA BUNGE NA URATIBU

JARIDA LA MTANDAONI TOLEO LA KWANZA
Januari 2024



Viongozi wa dini waombwa kuweka mkazo katika kusimamia maadili.

KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 BARABARA YA POSTA 40412 DODOMA TANZANIA
www.pmo.go.tz



Viongozi wa dini wameombwa kuendelea kusimamia imara na kukemea matendo maovu yanayopelekea mmomonyoko wa maadili hususan kwa vijana hasa katika mazingira ya yanayoendeshwa zaidi na ulimwengu wa kidijitali.

Hayo yamesemwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, (Sera, Bunge na Uratibu) Mhe. Jenista Mhagama wakati akimuwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt, Samia Suluhu Hassan katika Ibada Maalum ya Kuwekwa Wakfu Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, Dayosisi ya Mufindi, Mkoani Iringa.

Waziri amehimiza malezi bora kwa watoto na ikiwezekana jamii kurejea utamaduni wa kitanzania wa mtoto kulelewa na kuonywa na jamii nzima inayomzunguka.

"Serikali inatambua kuwa Viongozi wa dini wana mchango mkubwa katika kuwahimiza wananchi maadili mema na maisha ya uadilifu," Alifafanua

Waziri amenukuu maandiko Matakatifu kutoka Waraka wa Mtume Paul kwa Wagalatia Sura ya 6: 1-3 yanayosihi kuonya na pale inapobainika mmoja katika jamii amekwenda kinyume kwa kutenda kosa lolote.

Amewaaomba viongozi hao kueendelea kutekeleza jukumu hilo ipasavyo ili kulilinda Taifa dhidi ya janga la mmomonyoko wa maadili.

"Tunaamini kwa kupitia Imani yetu na kukua kwa kanisa, ni kukua kwa Imani ya dini, hivyo kutachochea maadili na kusaidia kupambana na vitendo vibaya vya rushwa na kuimarisha utawala bora" Alibainisha Aliendelea kusema kuwa, Mambo mazuri yatakayofanywa na washirika wa Dayosisi hiyo yataleta ari na chachu kwa watu wengine ambao sio wanashirika Dayosisi.

Waziri amesema kwamba licha ya Nchi ya Tanzania kutoegemea upande wowote katika masuala ya dini (Secular State) sehemu kubwa ya wananchi wanaamini katika Mungu kupitia dini na madhehebu mbalimbali.

Aidha, Alifafanua kuwa Serikali inaendelea kutambua uwepo wa dini nchini na umuhimu wake katika kulinda tunu za amani na utulivu pamoja na mchango mkubwa unaotolewa na taasisi za dini katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Waziri ametumia nafasi hiyo kupongeza na kushukuru Kanisa la Kilutheri Tanzania hasa kwa wale waliopata Dayosisi mpya na Mhashamu Askofu Mpya, kuwana matarajio makubwa sana kwa Dayosisi hiyo Mpya.

Kwa upande wake Askofu wa Jimbo la Mufindi Muhasham Baba Askofu Dkt. Anthony Kipangula, amesema kanisa linahitaji kushirikiana na Serikali kutoa elimu ya kujitegemea ili kusaidia vijana kupata ujuzi.

Alisema, Elimu ya Ufundi ni muhimu sana kwa vijana hasa wanaomaliza elimu ya msingi bila kwenda sekondari na wanaomaliza elimu ya sekondari bila kwenda juu zaidi.

"Kanisa linajipanga kuendeleza elimu ya ufundi katika chuo chetu cha Mafinga Lutheran vocation centre ikiwezekana kuanza mchepuo ufundi kama tawi la chuo kikuu kisaidizi cha Iringa," Alisema Baba Askofu.



## TAHOA yakabidhi zaidi ya Milioni 47 za ununuzi wa vifaa vya ujenzi kwa waathirika wa maafa ya Hanang

Jumuiya ya Kampuni za Uwindaji wa Kitalii Tanzania (Tanzania Hunting Operators Association-TAHOA) imetoa salamu za pole jamii ya Wana Hanang waliopatwa na maafa yaliyosababishwa na maporomoko ya tope na mawe kutoka mlima Hanang mkoani Manyara na kusababisha vifo, majeruhi, uharibifu mkubwa wa miundombinu na mali..

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo hii leo Januari 04, 2024 katika Ukumbi wa Mikutano wa JNCC Jijini Dar es Salaam Makamu Mwenyekiti wa TAHOA, Abdulkadir Mohamed amesema kuwa michango waliotoa ni michango iliyotolewa na makampuni ya uwindaji kwa namna walivyoguswa na ni kwa ajili ya kununua vifaa vya ujenzi wa nyumba za waathirika wa maafa hayo.

Alieleza kuwa, umoja huo umechanga fedha za kununua vifaa vya ujenzi vyenye gharama ya shilingi shilingi za Kitanzania milioni 47,409,800 ambavyo vitapelekwa Hanang.

"Sisi kwa umoja wetu tumechanga fedha za ununuzi wa vifaa vya ujenzi ambavyo vitapelekwa Hanang hivyo

"Sisi kwa umoja wetu tumechanga fedha za ununuzi wa vifaa vya ujenzi ambavyo vitapelekwa Hanang hivyo tumeungana na Serikali kwa kuamua kukabidhi mchango wetu utakaosaidia wananchi wa Katesh Hanang kurejesha hali zao za maisha katika ubora zaidi," alisema Abdulkadir

Akitoa neno la Shukrani mara baada ya kupokea msaada huo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Sera, Bunge na Uratibu, Mhe. Jenista Mhagama aliishukuru kampuni ya TAHOA kwa namna walivyojitoa kuungana na Serikali na kazi kubwa iliyofika huku akisema kuwa kazi kubwa iliyopo ni kurejesha hali hasa makazi kwa wana Hanang.

"Mmekuja wakati sahihi kwa kuzingatia mahitaji yaliyopo ni vifaa vya ujenzi, hivyo mmeleta msaada huu utasaidia vitu muhimu vinavyohitajika kwa ujenzi ikiwemo saruji ambayo itasaidia kupata makazi salama na sahihi kwa Wana Hanang", alieleza Mhe. Mhagama.

.

Kwa upande wake Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Angellah Kairuki amewashukuru TAHOA kwa kuonesha utayari wao wa kuweza kuchanga kwa ajili ya waathirika wa maafa ya Hanang huku akieleza kuwa zoezi lote limefanikiwa kutokana na uongozi mahiri wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan huku akitoa wito kwa wadau wengine kujitokeza kuungana na watanzania waliofikwa na maafa hayo.

"Kipekee nikupongeze Waziri mwenye dhamana ya uratibu, Mhe. Mhagama kwa namna umelisimamia hili na kuhakikisha hali za wakazi wa Hanang zinarejea, hakika mmefanya kazi kubwa sana kwa maeleklezo ya Mheshimiwa Rais wetu," alisisitiza Waziri Kairuki

.



## Serikali yaahidi kuendelea kurejesha hali katika miundo mbinu ya barabara iliyoathirika na Mvua

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulika na Sera, Bunge na Uratibu Mhe, Ummy Nderiananga amepongeza Kamati ya Maafa ya Mkoa wa Dar es salaam kwa jitihada mbalimbali za kurejesha hali katika maeneo ambayo miundo mbinu ya barabara imeathirika kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha.

Kauli hiyo ameitoa wakati wa ziara yake Mkoani humo alipotemebelea na kujionea athari za mvua zilizonyesha usiku wa kuamkia tarehe 20/ januari/2024 na kuathiri maeneo mabalimbali ya wilaya ya Kindondoni, Temeke, Kigamboni, Ubungo na Jiji la Ilala.

Naibu Waziri Ummy alisema anampongeza Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Abert Chalamila kwa uongozi ambao wameuonesha katika kurejesha halina kazi waliyofanya.

“Naomba tufanye kazi hii usiku na mchana ili tuweze kurejesha hali mapema bila kuathiri shughuli za biashara na shughuli

Sisi kama serikali tunawahakikishia wana Dar es salamu kwamba tutafanya kazi hii ya urejeshaji wa hali kwa nguvu bila kuchoka,

Naye Mkuu wa wilaya ya Kindondoni Mhe. Saad Mtambule amesema kazi waliyofanya ni kusimamia usafishaji wa mitaro na usawishaji wa mito na hivyo kusaidia maji kutotuwama kwa muda mrefu.

"Tumeendelea kuwaeleza wananchi walio katika maeneo ya pembezoni mwa mito kama; Mto Nyakasangwa, Mto Mpiji, Mto Tegeta, Mto Mlalakuwa na Mto Ng'ombe kuhamia maeneo ya juu ili kuepeuka athari za mvua,"alibainisha

Ujenzi wa nyumba holela umesababisha Watu kujenga mpaka kwenye mapito asili ya maji na kusababisha maji kukosa sehemu za kupita na kuingia maeneo ya watu

"Lakini pia tuna kazi ya kuendelea kuwaelimisha wananchi ili wafuate misingi ya ujenzi wa maeneo kulingana na ramani ya mipango Miji," alisisitiza

Akizungumza katika ziara hiyo Mkazi wa Ununio Bw. James Koyi ameishukuru serikali kwa kazi kubwa inayofanya ya urejeshajji wa hali katika maeneo yaliyoathirika mafuriko kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha mkoa wa Dar es salaam.

Hakuna aliyejua kama mvua itanyesha masaa ishirini na nne hata hivyo serikali iendelee kufanya kazi katika kurejesha hali, alisema.





Serikali yatoa misaada ya kibinadamu kwa waathirika wa mafuriko Kilimanjaro

Serikali imetoa misaada ya vyakula, magodoro, ndoo, madumu na mablanketi kwa kaya 119 za Kata Nane za Halmashauri ya Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro zilizokumbwa na mafuriko kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha.

Akikabidhi misaada hiyo ambyao ni mahindi tani 20, magodoro 150, mablanketi 300, ndoo 150, madumu 150, na mikeka 300 Naibu Waziri Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Mhe. Ummy Nderiananga amesema kuwa, Serikali inatambua changamoto iliyowakumba wananchi hao kutokana na mvua zilizonyesha na kusababisha mafuriko.

Katika hatua nyingine Naibu Waziri huyo ametumia nafasi hiyo kutoa onyo kwa baadhi ya watu wanaotoa

taarifa za uongo kupitia mitandao ya kijamii kucha mara moja tabia hiyo kwani wanasababisha taharuki.

"Inapotokea taarifa za maafa wapo wasemaji wake kwa mkoa ni Mkuu wa mkoa

na wilaya ni Mkuu wa wilaya sasa wapo watu wanarekodi na kusambaza taarifa za uongo kwenye mitandao na kusababisha taharuki kubwa niwaombe achaneni na hii tabia tumieni mitandao vizuri," Alisema Naibu Waziri Ummy.

Vile vile Naibu Waziri huyo ameiagiza Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Moshi kukutana na kamati ya maafa ya Wilaya pamoja na wataalam wengine ili kuweka mikakati ya uzibuaji wa njia za mto Nanga na mto Manguvu ili kuzuia mafuriko katika Kijiji cha Saningo, Kata ya Old Moshi.

Kwa upande wake, Mbunge wa Jimbo la Moshi Vijijini, Mhe. Prof. Patrick Ndakidemi alitumia nafasi hiyo kuishikuru Serikali chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo wamezikimbilia familia za waathirika wa mafuriko katika maeneo mbalimbali ikiwemo Wilaya ya Hanang mkoani Manyara.

Prof. Ndakidemi alisema kuwa, katika maafa hayo yaliyosababishwa na mvua jumla ya watu watano walifariki dunia pamoja na mashamba na vitu mbalimbali vikiwemo vyakula kusombwa na mafuriko.

"Msaada uliotolewa na serikali utasaidia kuzifariji familia ambazo zimekumbwa na mafuriko pamoja na kuwafariji watu ambao ni waathirika hatua hii ni kuonyesha jinsi ambavyo Serikali inawathamini" Alisema Prof. Ndakidemi.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Hai Mhe. Amir Mkalipa akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Moshi aliutaka uongozi wa Halmashauri kuhakikisha wanagawa vitu hivyo kulingana na maelekezo ya serikali na yeyote atakayekiuka hatosita kumchukulia hatua.

Kwa upande wao waathirika waliishukuru Serikali kuwajali wananchi wake wakati wote wanapokumbwa na changamoto hatua ambayo huwapa faraja na kusaidia kurejesha hali.



**“Wananchi fuatilieni taratibu na maelekezo ya serikali kukabiliana na madhara yatokanayo na mvua” Dkt. Yonazi**

Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Dkt. Jim Yonazi amewataka wananchi kuzingatia na kufuata taratibu zinazotolewa na Serikali ili kuweza kukabiliana na madhara yatokananyo na mvua hasa za El nino kuweza kuokoa maisha na mali zao. Ameyasema hayo Jijini Mwanza alipokuwa katika ziara ya kukagua hali ya Mafuriko katika Jiji la Mwanza ambapo mvua la El nino zinazoendelea zimeleta athari mbalimbali na kuharibu miundombinu pamoja na mali za watu.

Dkt. Yonazi amesema ni muhimu sana wananchi kuwa wazalendo na kufuata maelekezo ya serikali kwa sababu suala zima la uokoaji ni gharama.

"Suala hili ni gharama kwa Serikali lakini pia inaweza kugharimu maisha hivyo ni muhimu sana pale ambapo tumeelekezwa na Serikali kufuata taratibu tuweze kufuata taratibu." Alisisitiza.

Katibu Mkuu Dkt. Yonazi amebainisha kuwa kwa wananchi ambao wameelekezwa kuhama katika maeneo hatarishi waweze kuhama ili waweze kulinda maisha yao, mali zao na maisha ya jamii kwa ujumla na ametoa wito kwa wananchi kote nchini kufuata taratibu, miongozo na maelekezo halali ya Serikali na ndiyo namna ya kujilinda dhidi ya mafuriko na majanga.

Amewataka pia wananchi kushiriki katika miradi mikubwa akitolea mfano mradi wa ujenzi wa kingo za mto Nyamilongo unaopita katika wilaya ya Nyamagana ili maji yake yasiende katika makazi ya watu na kuharibu mali nyingine na kufahamu kwamba ushiriki wao utaleta faida katika maana ya kutunza mali zao, mali za asili na kuhakikisha kwamba maisha yanaendelea vizuri.

Katika hatua nyingine,Dkt. Yonazi amewaasa watumishi wa umma kufuata utaratibu hasa katika kusimamia suala zima la ujenzi holela, kwani unapofanyika ujenzi holela ni rahisi sana kupata madhara.

"Ili kuweza kuwa na makazi bora kwa wananchi wetu ni vizuri kuhakikisha maisha hayahatarishwi na mafuriko na hata yanapotokea mafuriko inakuwa rahisi kuokoa." Amesema Dkt. Yonazi

Kwa upande wake Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza Bw. Balandya Elikana amesema, mvua hizi za El nino kwa baadhi ya maeneo katika mkoa wa Mwanza zimeleta uharibifu wa baadhi ya miundombinu kama vile madaraja na Barabara

Aidha amepongeza Wakala wa Barabara vijijini na Mijini (TARURA) mkoani Mwanza kwa kuendelea kufanya kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba miundombinu hiyo inarejea katika hali yake ya kawaida.



Wabunge wakoshwa na uratibu wa maafa nchini

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria imeipongeza Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu kwa Usimamizi mzuri wa kukabiliana na Maafa nchini.

Pongezi hizo zimetolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Joseph Mhagama wakati wa wasilisho lililohusu namna Serikali ilivyojipanga katika kukabiliana na maafa pamoja na mfumo wa usimamizi wa Uratibu wa maafa katika kuzuia na kupunguza madhara ya majanga.

Pia wamepongeza Mpango wa Ujenzi wa Vituo vya utoaji huduma za matibabu kwa waraibu wa Dawa za kulevya nchini lililowasilishwa na Waziri wa Nchi ofisi ya Waziri Mkuu Sera,Bunge na Uratibu Mhe. Jenista Mhagama Bungeni Jijini Dodoma.

Mwenyekiti huyo alisema Serikali ilifanya kazi kubwa na ya kupongezwa kutokana na jitihada zilizofanyika kuhakikisha waathirika wa mafuriko katika Halmashauri ya Wilaya ya Hanag mkoani Manyara wanaokolewa na kurejesha hali.

“Tunapongeza sana Uongozi wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Serikali kwa ujumla kazi mliyofanya ni kubwa ya kuokoa maisha ya wananchi na mal zao licha ya baadhi yao kupoteza maisha kama kamati tunawapongeza sana,"Alisema Mwenyekiti wa kamati hiyo.

Mhe. Dkt. Mhagama alisema, inatia moyo sana kuona Wizara ama idara inazozisimamia zinafanya kazi ambazo watanzania wanazitarajia kwa hiyo kamati nayo inajiskia kama ni sehemu ya hayo mafanikio makubwa yaliyopatikana.

“Maafa ni majanga lakini tunapokabiliana nayo na kuyafanyia kazi vizuri inatupa nguvu sasa, tunapenda tukupongeze Mhe. Waziri Jenista Mhagama, Katibu Mkuu Dkt. Jim Yonazi na Watendaji wako wote kwa moyo wa uzalendo mliouonyesha katika kipindi kigumu ambacho Taifa lilipitia," Alieleza Mhe. Dkt. Mhagama.

Vilevile Kamati pia ilipongeza Mamlaka ya Kudhibiti na Kukabilana na madawa ya kulevya kwa kazi nzuri inayofanya ya kujenga vituo vya Urehebu na kushauri kujengwa vituo zaidi kwa Mikoa ya kusini pamoja mapambano ya uzalishaji na biashara ya Dawa za kulevya kama vile Bangi,Mirungi na dawa nyingine.

Akitoa maoni Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Mhe. Edward Olekaita Kisau, alifafanua kwamba namna Serikali ilivyokabiliana wakati wote wa maafa na baada ya maafa ili kuhakikisha inarejesha hali na shughuli kuendelea kama ilivyokuwa awali na janga la Hanang' ni mfano mzuri unaoweza kuchukuliwa katika uratibu mzima wa masuala ya kukabiliana na majanga nchini.

Naye Mjumbe wa kamati hiyo Mhe. Dkt Alice Kaijage akitoa maoni kuhusu wasilisho la Utekelezaji wa Mpango wa Ujenzi wa Vituo vya Utoaji wa Huduma za Matibab kwa Waraibu wa Dawa za Kulevya nchini alibainisha kuwa ni wakati mzuri sasa kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za kulevya (DCEA) kuongozewa fedha za maendeleo.

Jarida la Mtandao limeandaliwa na kutolewa na
kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu.



KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 MTAA WA RELINI , S.L.P 980
40480 DODOMA
Baruapepe, ps@pmo.go.tz, simu, +255262322480
Fax;255262324534, Tovouti;www.pmo.go.tz